

# KIELELEZO CHA JAMII

**Kielelezo hiki kitaipa jamii maelezo zaidi na kuisaidia kujiandaa  
kulinda haki zao.**

## NINI KILIFANYIKA?

Mnamo tarehe 8 Novemba 2016, Donald Trump alichaguliwa kuwa rais wa Marekani . Alichukua hatamu za uongozi tarehe 20 Januari 2017.

## JE, TUNAJUA NINI?

Donald Trump alifanya kampeni zako kwa msingi wa kutowapenda na kuwachukia wahamiaji. Tunajua kwamba jamii hii ina wasiwasi. Hatujui kwa uhakika kile Donald Trump atafanya, lakini tungependa kukufahamisha kwamba **tupo nawe** kupigania na kutetea haki zetu. Tuko pamoja.

## SASA TUFANYEJE?

**Utapata maelezo zaidi katika kielelezo hiki:**

- Zungumza na wakili wa uhamiaji kuhusu kesi yako
- Fanya mpango kuhusu jinsi hali hizi zinavyoweza kuathiri familia yako
- Jifunze kuhusu haki zako
- Piga ripoti kuhusu makosa ya chuki
- Pata maelezo kuhusu kile jiji lako linafanya kulinda jamii zetu
- Tahadhari na walaghai!

# MTOTO WAKO ANA HAKI YA KWENDA SHULE



Shule haiwezi kuuliza  
kuhusu hali ya uhamiaji  
ya mtoto au ya familia

Ni kinyume cha sheria kwa shule  
kukubagua wewe au mtoto wako  
kwa sababu ya hali yako ya  
uhamiaji, nchi ulikozaliwa, dini,  
asili, au rangi.



Ikiwa mtoto wako  
anahitaji usaidizi  
kujifunza Kiingereza, ana  
haki ya kupata mpango  
maalum wa kumsaidia



Una haki ya mtoto wako kuwa na mkalimani au  
mtafsiri kama sehemu ya elimu yake.





## TAARIFA MUHIMU KUHUSU HUDUMA ZA AFYA

Una haki ya kupata huduma za afya bila kujali ni nani  
rais wa Marekani.

Huduma za afya ni salama kwa ajili  
ya wakazi wote wa New York.

Watoa huduma za afya  
hawatafuatilia hali ya uhamiaji ya  
wagonjwa.

Una haki ya kupata usaidizi wa  
lughu na wa kifedha kutoka kwa  
kila mhudumu wa afya  
unayemtembelea New York.

Ikiwa una sifa stahiki, jisajili katika  
mipango ya umma au aua ya binafsi  
ya afya.

Piga simu **855-355-5777** ili  
uzungumze na mshauri wa masuala  
ya afya.

Zahanati na hospitali za kaunti na za  
umma ni chaguo la huduma za hali ya  
juu kwa bei nafuu kwa watu wote  
wanaoishi New York, bila kujali hali  
zao za uhamiaji.

# MAOFISA WA MLANGONI KWAKO...

## USIWARUHUS U WAINGIE BILA WARANTI

Sawa na walivyo maofisa wa polisi, maofisa wa Uhamiaji hawawezi kuingia kwako bila waranti iliyotiwa saini na jaji.

- Usiwhali kufungua mlanga
- Waombe wapitishe waranti chini ya mlanga au isimamishwe kwenye dirisha
- Thibitisha kwamba waranti ina jina lako
- Hata kama maofisa wa Uhamiaji wana waranti, kama lina jina la mtu usiyemjua au mtu aliyekuwa akiishi kwako, hawawezi kuitumia kuingia kwako



### Ikiwa hawana waranti

Ikiwa maofisa wa Uhamiaji hawana waranti au ikiwa waranti ni ya mtu mwininge usiyemjua au mtu asiyeshi kwako, waambie kwamba huwezi kuwaruhusu waingie bila kibali, au kwamba mtu wanayemtafuta haishi kwako, waombe kwa unyenyekevu kuondoka.

Ikiwa wanamtafuta mtu unayemjua, huna haja ya kuwaambia mahali mtu huyo yuko, waambie wakupe anwanu ya kuwasiliana nao, kisha uwaombe waondoke.

### ikiwa wana waranti

Hata kama maofisa wa Uhamiaji wana waranti, bado una haki zako!

Usiwaambie chochote, sema:

**“NIMEAMUA  
KUTUMIA  
MAREKEBISHO YA  
TANO YA SHERIA  
NA NINA HAKI YA  
KUWA KIMYA.”**

- Endelea kusema hivyo wakiamua kukupuuza.
- Usisaini hati zozote walizo nazo. Ni vyema kushauriwa na wakili kila wakati kama ni sawa kutia saini hati yoyote.
- Usiwape maofisa wa Uhamiaji hati yoyote inayokutambulisha kutoka nchi yako kama vile pasipoti yako.

### ikiwa watakukamata wewe au watu wengine

Ikiwa maofisa wa Uhamiaji wana waranti na watakukamata wewe au watu wengine kwako, usitie hati yoyote saini wala kukubali jambo lolote.

- Kaa na namba ya simu ya wakili unayeweza kumpigia.
- Hakikisha umeficha namba na hati muhimu sehemu salama nyumbani kwako, ambapo wanafamilia au marafiki wanaweza kuzipata ili kukusaidia.

### rekodi mawasiliano yenu


Hakikisha mtu mwininge aliye nawe nyumbani anarekodi matukio kwa video au sauti akitumia simu au kifaa kingine. Maofisa wa Uhamiaji wanapoondoka, wewe au mwenzako anaweza kuandika kila kitu anachokumbuka: maofisa wa Uhamiaji walivyo kuwa wamevalia, gari walilokuwa nalo, kilichotokea.

### ripoti hali ilivyokuwa

Ripoti mara moja kwamba maofisa wa Uhamiaji walikuja kwako.

Kama unaishi katika Jiji la New York, piga simu kwa Asasi ya Kulinda Wahamiaji (Immigrant Defense Project):  
**212-725-6422**

Kama unaishi nje ya Jiji la New York, piga simu kwa United We Dream:  
**1-844-363-1423**



# MAOFISA WA BARABARANI...

## waulize kama unaweza kwenda

Maofisa wa Uhamiaji wakikusimamisha barabarani na kukuuliza maswali, waulize moja kwa moja kama unaweza kwenda.

Wakikuambia ndiyo, waambie hutaki kujibu maswali yao na endelee kuenda.

Wakisema huwezi kwenda, waambie:

**"NIMEAMUA  
KUTUMIA  
MAREKEBISHO YA  
TANO YA SHERIA  
NA NINA HAKI YA  
KUWA KIMYA."**

## usikubali kukaguliwa

Usiruhusu maofisa wa Uhamiaji wakague vitu vyako au mifuko yako.

Waambie:

**"SIJAKUBALI  
UKAGUZI HUU."**

## usijibu maswali

Usijibu maswali kuhusu hali yako ya uhamiaji au mahali nchi ulikotoka. Waambie una haki ya kuwa kimya.

## usiwaonyeshe hati zako

Usiwaone hati zozote zinazoweza kukutambulisha kutoka nchini mwako (kwa mfano pasipoti yako).

## ripoti ulichoshuhudia

Ripoti moja kwa moja kwamba maofisa wa Uhamiaji walikusimamisha.

Kama unaishi katika Jiji la New York, piga simu kwa Asasi ya Kulinda Wahamiaji (Immigrant Defense Project):

**212-725-6422**

Kama unaishi nje ya Jiji la New York, piga simu kwa United We Dream:  
**1-844-363-1423**


Kusimamishwa na maofisa wa Uhamiaji kunaweza kuhofisha sana, lakini usikimbie au kutoroka, usiwape hati za uongo na usiseme uongo kamwe!



# UKISHUHUDIA MAOFISA WA UHAMIAJI WAKIMSHIKA MTU AU WAKIMVAMIA...

## rekodi tukio hilo

Una haki ya kupiga picha na kurekodi tukio hilo. Fanya hivyo kutoka umbali salama ili usifanye hali ya kukamatwa au kuvamiwa kuwa mbaya.



## nakili

Andika

- ni maofisa wangapi wamehusika
- namba za beji zao (kama unaweza kuona)
- mavazi yao na kile kilichoandikwa kwenye sare au vesti zao
- gari walilokuwa nalo (pamoja na namba ya usajili).

## ripoti ulichoshuhudia

Ripoti ulichoshuhudia moja kwa moja!

Kama unaishi katika Jiji la New York, piga simu kwa Asasi ya Kulinda Wahamiaji (Immigrant Defense Project):

**212-725-6422**

Kama unaishi nje ya Jiji la New York, piga simu kwa United We Dream:  
**1-844-363-1423**

# Ikiwa Una Wakili

## NI SHARTI WAKILI WAKO....

1. Akufafanulie sheria na chaguo ulizo nazo
2. Akufahamishe kuhusu kesi yako na tarehe au miadi yote ya mahakamani
3. Atie saini kwenye karatasi zote anazoandaa na kuwasilisha kwa serikali kwa niaba yako
4. Akupe nakala za karatasi zote anazowasilisha kwa serikali (hata kama una deni lake)
5. Afafanue kwa maandishi ada zote anazotoza kwa ajili ya huduma
6. Ajibu simu na barua pepe zako kwa upesi
7. AKUHESHIMU kila wakati
8. Aweke taarifa zako kwa siri



## Una haki ya:

- KUOMBA ithibati ya kufuzu kwake
- KUPEWA risiti kwa pesa zozote unazolipa  
(*Tumia hundi au hawala ya pesa KILA WAKATI*)
- Kumwachisha kazi wakili wako na kumtafuta mwingine
- Una haki ya **kupata nakala** ya maombi au hati zozote zinazohusiana na uhamiaji

## USIHADAIWE

### Usiwahi Kulipa kwa PESA TASLIMU

- Lipa kwa Hundi au Hawala ya Pesa  
**KILA WAKATI!!!**

## PATA USAIDIZI!!

Fungua [www.protectingimmigrants.org](http://www.protectingimmigrants.org)

PIGA SIMU ya Moja kwa Moja kwa  
Wamarekani Wapya  
(800-566-7636)

- Pata mwanasheria au wakili asiyelipiza au anayetoza ada nafuu
- Pokea maelekezo ya kupata asasi za kiraia

## WAKILI WAKO KAMWE HATAKIWI:

1. Kukosa kufika mahakamani au katika mahojiano yako bila kukufahamisha mapema
2. Kukushawishi UDANGANYE
3. Kukuomba utie saini kwenye fomu zisizo na kitu au kusaini fomu zilizo na maelezo ya uongo
4. Kuweka hati zako asili
5. Kukuomba uwasilishe hati ghushi



Fomu zote za uhamiaji BILA MALIPO:

[www.uscis.gov](http://www.uscis.gov)

EPUKA ULAGHAI

SOMA HATI ZOTE KWA MAKINI  
kabla ya kutia saini

KAMWE USIWAHI KULIPIA AU  
KUSAINI Fomu za Uhamiaji zisizo  
na maelezo au ZENYE MAELEZO  
YA UONGO

USIMWACHIE mtu yeyote hati  
zako asili

Toa nakala ya hati zako kila  
wakati

## KUPATA USAIDIZI WA UHAMIAJI

- Wanasheria na wawakilishi waliodhinishwa na Bodi y a Rufaa za Wahamiaji (BIA) pekee ndio wanaoweza kutoa ushauri wa sheria
- Kamwe usimlipe “Notario”, wakala wa usafiri, mtayarisha kodi, au mwandaa fomu ili akuambie ni fomu gani unahitaji au akusaidie kuandaa fomu hizo
- Kujaza ombi lisilo sahihi si kupoteza pesa tu—inaweza kufanya ufukuzwe nchini

## IKIWA UNASHUKU KWAMBA SI KWELI, UWEZEKANO NI KWAMBA SI KWELI!!!!

- **WALAGHAI** huahidi wahamiaji manufaa ambayo huwezi hustahiki kupata, lengo ni kupata pesa zako!
- Wanasheria na wawakilishi waliodhinishwa na BIA **wanatakiwa kuwa wakweli, hata wanapowasilisha habari mbaya**